

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

640


**HISABATI**

**Muda: Saa 3**

**Jumatano, 08 Mei 2019 asubuhi**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka kila sehemu B na C.
3. Sehemu A in alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi, vikokotozi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



1



## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

- (a) Nini maana ya sehemu katika somo la Hisabati?

(b) Ipi ni kubwa kati ya  $\frac{1}{2}$  na  $\frac{2}{3}$ ?
- Badili vipimo vifuatavyo;

(a) Sentimita 2700 kuwa mita

(b) Lita 120 kuwa mililita.
- (a) Nini maana ya utunzaji wa vitabu vya fedha?

(b) Taja faida mbili za kutunza vitabu vya fedha.
- (a) Andika namba 35.997 katika nafasi mbili za desimali.


(b) Kadiria 889113 katika maelfu yaliyo karibu.
- Andika namba mbili zinazofuata katika mfululizo ufuatao:

(a) 4, 2, 0, -2, \_\_\_\_\_, \_\_\_\_\_.

(b)  $\frac{1}{3}$ ,  $\frac{1}{6}$ ,  $\frac{1}{12}$ ,  $\frac{1}{24}$ , \_\_\_\_\_, \_\_\_\_\_.
- Tafuta kigawe kidogo cha shirika cha 4, 6 na 8 kwa njia ya kuorodhesha.
- Rahisisha:

(a)  $4\frac{1}{13} : 7\frac{3}{13}$

(b) km130 : km160.
- Tafuta thamani ya  $R$  katika duara lifuatalo ikiwa  $AB$  ni kipenyo chake.



9. Eleza umuhimu wa kuandaa andalio la somo kwa mwalimu wa somo la Hisabati.
10. Taja matumizi manne ya namba kamili katika maisha ya kila siku. Toa maelezo mafupi kwa kila hoja.

### SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

11. Jedwali lifuatalo linaonesha alama za wanafunzi katika jaribio la Hisabati Darasa la Saba. Soma kwa makini taarifa za jedwali hili na kujibu maswali yanayofuata;


Alama (%)	35	30	45	50	60	70	80
Idadi ya Wanafunzi	2	3	6	14	5	8	2

- (a) Je, alama gani ni ndogo zaidi?
- (b) Je, alama ipi ni kubwa zaidi?
- (c) Je, alama gani ambayo wanafunzi wengi zaidi walipata?
- (d) Ikiwa asilimia 50 ilikuwa alama ya ufaulu, ni wanafunzi wangapi walifaulu jaribio?
- (e) Wanafunzi wangapi walifeli jaribio?
- (f) Je ni wanafunzi wangapi walifanya jaribio?
12. Rahisisha mitajo ifuatayo:
- (a)  $2\frac{2}{5} + 2\frac{1}{10}$
- (b)  $2\frac{1}{3} + 3\frac{4}{5}$
- (c)  $\frac{1}{2} - \frac{1}{3}$
13. Katika mkutano wa wanakijiji, kuna wakulima 20 na wafanyakazi 15. Iwapo wanakijiji 7 ni wakulima na pia ni wafanyakazi; wanakijiji 2 si wakulima wala wafanyakazi. Tumia kanuni kutafuta idadi ya;
- (a) wanakijiji waliohudhuria mkutano.
- (b) wanakijiji ambao ni wakulima tu.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

14. (a) Onesha jinsi ya kutafuta thamani ya  $x$  katika mchoro ufuatao kwa wanafunzi wa Darasa la Saba:



- (b) Tumia michoro kuonesha namna utakavyomfundisha mwanafunzi wa Darasa la Kwanza kukokotoa:

(i)  $7 - 5 = 2$ .

(ii)  $5 - 5 = 0$ .

(Usitumie michoro ya sinia la namba au abakasi).

15. Kwa kutumia mifano, onesha zana halisi au vifaa vya kufundishia na kujifunzia jinsi ya kupata  $\pi$ , na kuthibitisha kuwa mzingo wa duara  $C = \pi d$ , ikiwa  $d$  ni kipenyo cha duara kwa mwanafunzi wa Darasa la Sita.

16. (a) Eleza maana ya pembe tatu mraba.

- (b) Kwa kutumia kielelezo cha pembe mraba, onesha utakavyothibitisha kanuni ya Pythagoras kuwa  $a^2 + b^2 = c^2$ .